



OFISI YA RAIS,
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM
(BARUA ZOTE ZIPELEKWE KWA MKURUGENZI WA JIJI)



Tarehe: 24 Agosti, 2020

TAARIFA KWA UMMA

**WAFANYABIASHARA WATAKIWA KUFANYA MAANDALIZI YA KUTOA HUDUMA
KITUO KIPYA CHA MABASI DAR ES SALAAM**

Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, ambayo inasimamia ujenzi wa kituo kipya cha mabasi ya abiria kinachojengwa katika eneo la Mbezi Luis katika Manispaa ya Ubungo jijini Dar es Salaam, sasa inawajulisha rasmi wananchi kwamba imeanza kufanya maandalizi ya kuwakaribisha wafanyabiashara mbalimbali ndani ya kituo hicho chenye uwezo wa kuwahudumia mabasi 3,456 kwa siku.

Kituo hicho kinachojengwa kutokana na fedha za ruzuku kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya miradi ya kimkakati kutoka Serikali ya Awamu ya Tano ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, chini ya uongozi wa Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli, kwa gharama za shilingi bilioni 50.9 na fedha za mapato ya ndani ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam katika awamu ya kwanza kinatarajiwa kuwa kituo cha kwanza cha kisasa chenye hadhi ya kimataifa katika ukanda wa Afrika Mashariki. Kituo hicho kitakachotoa huduma ya usafiri wa abiria ndani na nje ya nchi ujenzi wake hadi sasa umefikia asilimia 77 ambapo Halmashauri imefanikiwa kwa kiasi kikubwa kufikia malengo ya ujenzi wake.

Wakati hatua za kukamilisha ujenzi huo zikiendelea, Halmashauri ya Jiji kwa sasa ipo katika maandalizi ya kuwakaribisha wafanyabiashara mbalimbali kuomba maeneo ya kufanya biashara ndani ya kituo hicho. Hivyo, Halmashauri imeona ni vema kuwajulisha mapema wafanyabiashara wenye nia hiyo ili waweze kujiandaa kutumia fursa hiyo kutokana na mpangilio wa huduma zilizopangwa kutolewa katika kituo hicho.

Huduma zinazotarajiwa kutolewa katika kituo hicho ni maduka makubwa (Shopping Malls), migahawa, huduma za kibenki, huduma zitolewazo na makampuni ya simu na ofisi za kupangisha. Aidha, kutakuwa na eneo lililotengwa kwa ajili ya wafanyabiashara ndogo ndogo (Wamachinga), mama lishe na baba lishe, wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. Huduma zingine ni kituo cha afya, maegesho ya magari madogo, mabasi na malori, uoshaji wa magari na gereji kwa ajili ya utengenezaji magari. Halmashauri inawahamasisha wananchi kujiandaa kutumia fursa hiyo baada ya tangazo la zabuni kutolewa kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu za zabuni.

“Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli kwa ujenzi wa kituo hicho katika Jiji la Dar es Salaam kikiwa ni mojawapo kati ya miradi mingi mikubwa ya kimkakati ya Serikali ya Awamu ya Tano inayotekelezwa nchini kwa mafanikio makubwa”, anasema Mkurugenzi wa Jiji la Dar es Salaam, Sipora Liana ambaye pia anawakumbusha wananchi kwamba Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam bado haijaanza kupokea maombi ya fursa mbalimbali za biashara katika kituo hicho kipya. Maombi yote yatakayotumwa kabla ya tangazo la zabuni hayatafanyiwa kazi, hivyo anawataka wananchi kuepuka matapeli.


Gaston L. Makwembe

MKUU WA KITENGO CHA ITIFAKI NA UHUSIANO